ELIMU INAYOZINGATIA UMAHIRI
TATHMINI YA MWISHO WA MUHULA WA 3 2026

DARASA LA 4

KISWAHILI SHUGHULI ZA UTUNGAJI

MUDA: Dakika 40

JINA: _____NAMBARI YA AD: _____

SHULE: _____TAREHE: _____

MAAGIZO KWA WANAFUNZI

1. Soma kwa makini mada ya utungaji kabla ya kuanza kuandika.
2. Andika utungaji kuhusu **MNYAMA NIMPENDAYE SANA**
3. Panga mawazo yako kabla ya kuanza kuandika.
4. Utungaji wako uwe na **utangulizi, kiini na hitimisho** linalofaa.
5. Andika kwa kutumia sentensi kamili na zenye maana.
6. Panga mawazo yako katika aya zilizo wazi.
7. Tumia sarufi, tahajia na alama za uakifishaji kwa usahihi.
8. Tumia maneno ya kuvutia na yanayofaa kumwelezea rafiki yako wa dhati.
9. Andika kwa nadhifu na kwa uwazi.
10. Kagua kazi yako kwa makini na usahihishe makosa yoyote kabla ya kuikabidhi.
11. Usinakili kazi ya mwanafunzi mwingine.
12. Andika utungaji wako katika nafasi uliyopewa.

(Alama 20)

MNYAMA NIMPENDAYE SANA

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA

MWONGOZO WA KUSAHIHISHA
ELIMU INAYOZINGATIA UMAHIRI

TATHMINI YA MWISHO WA MUHULA WA 3 – 2026

DARASA LA 4

KISWAHILI – SHUGHULI ZA UTUNGAJI

MUDA: Dakika 40

MADA: MNYAMA NIMPENDAYE SANA

JUMLA: ALAMA 20

1. MAUDHUI – ALAMA 10

Mwanafunzi anatarajiwa kuandika kuhusu mnyama anayempenda. Majibu yanaweza kutofautiana kulingana na mnyama aliyechagua.

Vipengele vinavyoweza kutuzwa:

Kipengele	Alama
Kumtaja mnyama anayempenda	1
Kueleza mwonekano wa mnyama huyo	2
Kueleza anapoishi au kufugwa	1
Kueleza chakula anachokula	1
Kueleza tabia/namna anavyofanya	2
Kueleza sababu zinazomfanya ampende	2
Kutoa hitimisho linalofaa	1
Jumla	**10**

Kumbuka: Mwanafunzi anaweza kutoa hoja nyingine sahihi zinazohusiana na mada. Usimlazimishe kutumia hoja zilizoorodheshwa hapo juu.

2. MPANGILIO WA MAWAZO – ALAMA 3

Kipengele	Alama
Utangulizi unaofaa	1
Mawazo yamepangwa kwa mtiririko mzuri	1
Hitimisho linalofaa	1
Jumla	**3**

3. SARUFI NA UUNDAJI WA SENTENSI – ALAMA 3

Mwanafunzi atuzwe kulingana na uwezo wake wa:

- Kutumia sentensi kamili na zenye maana.
- Kutumia maneno kwa usahihi.
- Kutumia nyakati na viambishi kwa usahihi.
- Kuepuka makosa mengi ya kisarufi.

Jumla: Alama 3

4. TAHajia – ALAMA 2

Mwanafunzi atuzwe kwa:

- Kuandika maneno kwa tahajia sahihi.
- Kutumia herufi kubwa inapohitajika.
- Kuepuka makosa ya kuandika maneno.

Jumla: Alama 2

5. UAKIFISHAJI NA USAFI – ALAMA 2

Kipengele	Alama
Matumizi sahihi ya alama za uakifishaji	1
Usafi na mwandiko unaosomeka	1
Jumla	**2**

MUHTASARI WA MGAWANYO WA ALAMA

Eneo la Tathmini	Alama
Maudhui	10
Mpangilio wa mawazo	3
Sarufi na uundaji wa sentensi	3
Tahajia	2
Uakifishaji na usafi	2
JUMLA	**20**

MFANO WA UTUNGAJI UNAOWEZA KUPATA ALAMA NZURI

Mnyama Nimpedaye Sana

Mnyama ninayempenda sana ni mbwa. Nina mbwa mmoja nyumbani ambaye anaitwa Bruno. Bruno ana manyoya meusi na meupe. Ana miguu minne, mkia na masikio mawili.

Mbwa wangu huishi nyumbani kwetu. Mimi humlisha nyama, mifupa na chakula kingine kinachofaa. Bruno ni mnyama mtiifu na mwenye urafiki. Yeye hulinda nyumba yetu wakati wa usiku. Pia hupenda kucheza nami wakati ninapokuwa nyumbani.

Ninampenda Bruno kwa sababu ni rafiki yangu na hutulinda. Mimi humtunza vizuri kwa kumpa chakula, maji na mahali safi pa kulala. Kwa kweli, Bruno ni mnyama ninayempenda sana.

Mwalimu: *Mwanafunzi asitarajiwe kunakili mfano huu. Utungaji wake mwenyewe utathminiwe kwa kuzingatia mawazo na lugha aliyotumia.*

Kiwango	Alama	Maelezo
Muzidisha Matarajio	**16–20**	Mwanafunzi ameonyesha uwezo bora zaidi ya matarajio. Ameeleza mada kwa kina, mawazo yamepangwa vizuri, ametumia lugha sahihi, sarufi na tahajia nzuri, na kazi ni safi.
Kufikia Matarajio	**11–15**	Mwanafunzi ametimiza mahitaji makuu ya kazi. Ameeleza mada vizuri, mawazo yanaeleweka, ingawa kuna makosa machache ya sarufi, tahajia au uakifishaji.
Kukaribia Matarajio	**6–10**	Mwanafunzi ameonyesha uelewa wa kiasi lakini utungaji una mapungufu katika maudhui, mpangilio wa mawazo, sarufi, tahajia au uakifishaji.
Chini ya Matarajio	**0–5**	Mwanafunzi hajaonyesha uelewa wa kutosha wa mada. Mawazo ni machache au hayana mtiririko, na kuna makosa mengi ya lugha, tahajia na uakifishaji.